**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA UCHUMI YA BARAZA LA WAWAKILISHI, KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA YA KUANZISHA TAASISI YA WAHASIBU, WAKAGUZI NA WASHAURI ELEKEZI WA KODI ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwanza kabisa, napenda nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu mwenye kustahiki kushukuriwa na Viumbe vyote kwa kutujaalia uhai na afya njema na tukaweza kukutana hapa katika Baraza lako Tukufu kwa lengo la kuendelea kuwatumikia Wananchi wa Zanzibar kwa kutekeleza majukumu yetu mbali mbali kwa niaba yao ambapo leo tupo hapa kuupitia na kuujadili Mswada huu uliopo mbele yetu. Namuomba Mwenyezi Mungu anijaaliye ufasaha katika uwasilishaji wa Hotuba hii na atupe usikivu na uelewa ili hatimaye tuweze kuuchangia kwa umakini kwa maslahi ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,**

Nitakua mchoyo wa fadhila ikiwa nitashindwa kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako ili niweze kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi yanayohusu mswada wa sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri elekezi wa kodi zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa dhati kabisa nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa hatua anazozichukua katika kutetea maslahi ya Zanzibar, ikiwa ni pamoja na kupambana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi. Hivyo, mswada huu umekuja katika muda mwafaka na utasaidia sana kuondoa udanganyifu kwenye fedha za Umma. Sambamba na hilo, Kamati yangu inamshukuru Makamo wa kwanza wa Rais Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamo wa Pili Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla kwa ujasiri wao katika jukumu zima la kumsaidia Mheshimiwa Rais wa Zanzibar katika mapambano dhidi ya Rushwa na matumizi mabaya ya madaraka sambamba umahiri wao kwenye uendelezaji na uimarishaji wa sekta za Uwekezaji, Fedha na Uchumi.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba sasa nichukue fursa hii kuupongeza uongozi wa Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Fedha na Mipango hususan Mheshimiwa Waziri Dkt Sada Mkuya Salum kwa uongozi wake bora na jitihada anazozichukua kwenye suala zima la kupambana na wakwepa kodi, kwani Serikali bila ya kukusanya kodi haitaweza kutimiza azma yake kwenye kuleta maendeleo wananchi wake. Kamati pia inampongeza Naibu Waziri Mheshimiwa Ali Suleiman Ameir (Mrembo) kwa jitihada zake anazozichukua kumsaidia Mheshimiwa Waziri kwenye suala zima la kusimamia sera na mipango mbalimbali iliojiwekea wizara kwenye suala la kuhakikisha Zanzibar inapata maendeleo. Aidha, Kamati inawapongeza wasaidizi wake wakiwemo Katibu Mkuu, Naibu Katibu Wakuu na Wakurugenzi pamoja na watalaamu wengine wa

Wizara kwa mashirikiano na ufafanuzi waliyoutoa kwa Kamati yetu katika kipindi chote cha majadiliano ya Mswada huu.

**Mheshimiwa Spika,**

Napenda kuwashukuru Wanasheria wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa uchambuzi na ufafanuzi wa hoja mbali mbali zilizojitokeza wakati wa kuujadili mswada huu kwenye ngazi ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,**

Fasili ya (7) ya kanuni ya 84 ya Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2020 inaipa uwezo Kamati yetu kuwaalika Wadau mbali mbali kila inapotokea shughuli ya kujadili miswada ya sheria. Kwa heshima naomba niwataje wadau hao kama ifuatavyo:

1. Maisha Consultant
2. Imara Consultant
3. Zanzibar Association of Accountants and Auditors
4. Nasaha Consultant
5. Khans Consultant

Kamati inathamini mchango mkubwa wa Wadau hao na kuwashukuru kwa maoni na ushauri mzuri uliotuwezesha kuwa na mawanda mapana ya kuufahamu Mswada huu.

**Mheshimiwa Spika,**

Nitakuwa sijatenda haki iwapo sitowashukuru Wajumbe wa Kamati ya Uchumi kwa kazi nzito waliyoifanya ya kuujadili na kuuchambua mswada ulioletwa mbele yao kwa upeo na ustadi wa hali ya juu. Kwa heshima na taadhima, naomba sasa niwatambue kwa kuwataja majina yao Waheshimiwa Wajumbe wafuatao wa

Kamati ya Uchumi:-

1. Mhe. Sabiha Filfil Thani - Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt Soud Nahoda Hassan - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Panya Ali Abdallah - Mjumbe
4. Mhe. Hassan Hamad Omar - Mjumbe
5. Mhe. Rukia Omar Ramadhan - Mjumbe
6. Mhe. Ameir Abdalla Ameir - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,**

Katika uchambuzi wa Mswada huu, Kamati yetu ilifanya kazi na makatibu wetu wawili ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia na kuturahisishia kuuchambua ipasavyo mswada huu, naomba nao niwatambue kwa kuwataja majina yao kama ifuatavyo;

1. Ndugu Noman Thabit Noman -Katibu; na
2. Ndugu Asma Ali Kassim -Katibu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaamini kuwa uanzishwaji wa Taasisi hii hapa Zanzibar utasaidia kuongeza nafasi za ajira kwa vijana wetu kwa ngazi ya wataalamu, ambao wataweza kujiajiri wenyewe kama washauri elekezi wa kodi, wahasibu binafsi na wakaguzi ambapo watakuwa wanatoa ushauri wa kifedha na wa kikodi kwa Taasisi za Serikali, taasisi binafsi na hata mtu mmoja mmoja. Hali hii itawafanya waweze kupata kipato kutokana na ukubwa wa kazi waliokubaliana na wateja wao na kuwasaidia kujikimu wao na familia zao na kuiondolea Serikali mzigo wa vijana wanaosubiri ajira za Serikali. Tunaipongeza Serikali kwa kuibua chanzo kipya cha mapato kwani kila watakaolipwa wataalamu hao wa kodi na ukaguzi itawalazimu na wao kulipa kodi kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati yetu ina matumaini makubwa kwa vijana wa kizanzibari wanaomaliza masomo ya kodi na uhasibu kuwa wengi wao ni wenye tabia njema, waliolelewa kwenye misingi ya kidini na tamaduni za kizanzibar, ila wapo wachache wanaozitia doa fani hizo na ndio hasa wanaokusudiwa kwenye sehemu ya saba ya mswada ya huu ambayo imeweka adhabu kali sana kwa watakaojaribu kwenda kinyume na masharti yaliowekwa kwenye sehemu hiyo ya mswada.

**Mheshimiwa Spika,**

Kimsingi, Kamati yetu inakubaliana na dhana nzima iliyobebwa na mswada huu pamoja na marekebisho iliyoyapendekeza wakati ilipokaa na Wizara kwa ajili ya kuupitia mswada huu kwa nia ya kuujenga zaidi. Marekebisho hayo yamegawika katika sehemu mbali mbali zikiwemo makosa ya kiuandishi, makosa katika uteuzi wa maneno, makosa ya kukosekana kwa baadhi ya vitu muhimu na vya msingi kuwemo katika mswada huu hususan suala la tafsiri ya neno “**Mhasibu”au “Wahasibu**”ambao ndio walengwa wakuu wa Mswada huu.

**Mheshimiwa Spika,**

Mapendekezo ya Kamati yetu kwa marekebisho ya mswada huu ni kama yafuatayo:

1. K**ifungu cha 1** cha Jina Fupi na kuanza kutumika, Kamati inapendekeza kufutwa na kuandikwa upya kifungu hicho na kisomeke kama ifuatavyo:

   “Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Taasisi ya Wahasibu,

Wakaguzi na Washauri elekezi wa kodi Zanzibar, 2022 na itanza kutumika mara tu itakapotiwa Saini na Rais na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali”

2. Katika **Kifungu cha 2,** Kamati inapendekeza marekebisho katika tafsiri ya baadhi ya maneno.

   a) Kwa kufuta neno “ukaguzi” na kuweka tafsiri mpya ya neno hilo kama ifuatavyo:

      “**Ukaguzi”** maana yake ni kazi ya kuhakikisha yenye lengo la kupunguza hatari ya kazi ya kuhakiksha katika kiwango kidogo kinachokubalika kwenye mazingira ya kazi husika kama msingi wa maelezo yakinifu ya hitimisho la aliefanya ukaguzi;

   b) Kwa kuongeza tafsiri ya neno “**Muhasibu”**kama ifuatavyo;

      “**Muhasibu”**maana yake ni mtu aliesajiliwa na Taasisi kama mhasibu wa umma aliethibitishwa kufanya kazi za uhasibu.

3. **Kifungu cha 8,** Kamati inapendekeza marekebisho kama ifuatavyo:

   A. Kufutwa kifungu kidogo cha 2 na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

   Bodi itaundwa na:

   I. Mwenyekiti ambae atateuliwa na Rais,

   II. Mhasibu Mkuu wa Serikali,

   III. Mkurugenzi Mtendaji,

IV. Wajumbe watatu kila mmoja kutoka katika jumuia ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi na

V. Wakili wa Serikali Kutoka Afisi ya Mwansheria Mkuu.

B. Kufutwa kifungu kidogo cha 3 na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo:

"Isipokua Mwenyekiti, Mhasibu Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi Mtendaji, wajumbe wengine watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na Taasisi husika kwa kuzingatia mgawanyo wa kijinsia, Elimu na Uzoefu".

**Mheshimiwa Spika,**

Marekebisho mengine ya Mswada huu, yaliyofanywa na Kamati yetu, yameainishwa kwenye waraka wa marekebisho ambayo yameingizwa kwenye Baraza mtandao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa kumalizia naomba kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa umakini wa hali ya juu wakati wote nilipokua nikiwasilisha hotoba hii na ninawaomba Waheshimiwa wajumbe wa Baraza hili wauchangie mswada huu, wauchambue kwa kina na hatimae kuupitisha kwani hali tulionayo kwenye vita ya kupambana na wasiolipa kodi na wabadhirifu wa kifedha ni ngumu kwa sasa na Mswada huu ndo Muarubaini wake.

**HITIMISHO**
Mheshimiwa Spika,

Kwa niaba ya Kamati yangu, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Ahsante,

………………..………

Mheshimiwa Sabiha Filfil Thani,
Mwenyekiti,
Kamati ya Uchumi,
Baraza la Wawakilishi,
**Zanzibar**.